**Chanjo na Dozi ya Ziada ya COVID-19 Nyumbani Husaidia Kuboresha Ufikiaji na Usawa wa Afya**

Takriban asilimia 30 ya wakazi wa jimbo la Washington hawazingatiwi kama waliopokea chanjo kamili dhidi ya COVID-19. Data inaonyesha kuwa chanjo hulinda watu dhidi ya virusi. Chanjo hupunguza nafasi ya ugonjwa mkali na kifo ukipata virusi na kusaidia kupunguza idadi ya wanaolazwa hospitalini kwa sababu ya virusi. Ni muhimu kupata misururu asili ya chanjo na dozi ya ziada ili kusaidia kudhibiti mwitikio wa kingamwili yako dhidi ya aina mpya za COVID-19. Pendekezo la sasa la dozi ya ziada limeonyeshwa katika chati inayofuata:

| Chanjo iliyokamilishwa katika misururu ya msingi | Umri ulioidhinishwa kwa chanjo ya ziada | Kipindi kati ya dozi ya awali ya msingi (pamoja na dozi ya ziada, panapotumika) na dozi ya kiongeza nguvu | Idadi ya dozi |
|---|---|---|---|
| Pfizer-BioNTech | Miaka ≥ 12 | Miezi ≥ 5 | 1 |
| Moderna | Miaka ≥ 18 | Miezi ≥ 5 | 1 |
| Janssen | Miaka ≥ 18 | Miezi ≥ 2 | 1 |

Saidia kujilinda na kuwalinda wale ambao hawawezi kupokea chanjo. Watu wengi ambao hawawezi kutoka nyumbani wanawategemea wengine kusaidia kuleta mahitaji yao ya kila siku, pamoja na wengine wanaokuja kwa nyumba mara kwa mara. Wanaweza kudhurika kwa mfiduo wa virusi kutoka kwa wengine ambao huenda hawajapokea chanjo au bila kujua kuambukizwa kupitia usambazaji wa kijamii.

**Iwapo wewe au mtu unayemjua hawezi kutoka nyumbani na anahitaji chanjo ya COVID-19 au dozi ya ziada, iombe leo kupitia mojawapo ya chaguo zifuatazo:**

- Piga simu kwa mamlaka yako ya afya ya ndani ili kupata huduma za chanjo kwa wasiowenza kutoka nyumbani.
- Piga simu kwa Nambari ya Simu ya Dharura ya Usaidizi wa COVID-19 katika Jimbo ili kuwafahamisha kuwa unahitaji huduma za chanjo kwa asiyeweza kutoka nyumbani. Bofya 1-800-525-0127 au 1-888-856-5816, kisha ubonyeze #. **Ukalimani wa lugha unapatikana!**
- Kamilisha fomu ya usajili mtandaoni iliyounganishwa hapo chini ili kukuunganisha na kaunti inayopatikana na/au timu za chanjo katika jimbo wanaoweza kutoa au kupanga huduma za chanjo kwa wasioweza kutoka nyumbani.

Kiungo cha Uchunguzi wa Ombi la Chanjo kwa Wasioweza Kutoka Nyumbani cha Department of Health (DOH, Idara ya Afya): https://redcap.link/WA_HomeBasedVax (Kiingereza)

Ukiwa na maswali kuhusu huduma hii, tafadhali tuma barua pepe: covid.vaccine@doh.wa.gov.

**Historia ya Programu**

Department of Health (DOH, Idara ya Afya) ilianza kutoa chanjo kwa watu wasioweza kutoka nyumbani mnamo Machi 2021. Uchunguzi wa DOH wa Ombi la Chanjo kwa Wasioweza Kutoka Nyumbani (Kiingereza) unasimamia kaunti zote 39 katika jimbo la Washington. Watoaji chanjo katika eneo wanaendelea kutoa ufikiaji na huduma za kutoa chanjo za msingi na dozi za ziada kwa wanaohitaji. Huduma za chanjo kwa watu wasioweza kutoka nyumbani wanaweza kuombwa katika lugha za ziada kwa kupiga simu kwenye Nambari ya Simu ya Usaidizi wa COVID-19 (Piga 1-800-525-0127 au 1-888-856-5816), kisha bonyeza # ili kupata usaidizi wa lugha.

**Kuboresha Usawa wa Chanjo**

Huduma za Chanjo kwa Wasioweza Kutoka Nyumbani hutoa chanjo za COVID-19 katika maeneo ya jimbo ambapo chanjo vinginevyo haziwezi kupatikana. Lengo la huduma hizi ni kuboresha usawa wa afya na ufikiaji wa chanjo ya COVID-19 kwa wale ambao huenda:

- Hawawezi kutoka nyumbani, kupanga foleni, au kutembea umbali wowote.
- Wanapitia ulemavu wa kimwili au kiakili.
- Wanapitia hali za afya ya kiakili zinazobana ufikiaji.

Chanjo za watu wasioweza kutoka nyumbani husaidia kuboresha usawa wa afya katika maeneo ya jimbo yanayojulikana kama majangwa ya chanjo. Majangwa ya chanjo hutokea wakati ambapo mojawapo ya yafuatayo ni kweli:

- Hakuna maeneo ya chanjo.
- Hakuna wahudumu wa afya wanaotoa chanjo.
- Kuna watoaji wachache wanaopatikana kuhudumia eneo la kijiografia na watu waliopo.

Huduma za chanjo za umma huenda zisipatikane ah ziwe vigumu kufikia katika maeneo haya. Huduma ya chanjo kwa wasioweza kutoka nyumbani inatoa masuala ya ufikiaji ambayo hutokea mara kwa mara wakati wa kuishi katika maeneo ambayo ni vigumu zaidi kufikia na maeneo ya vijijini zaidi katika jimbo.

Huduma za chanjo za kutembeatembea husaidia kutoa ufikiaji kwa chanjo inayookoa maisha kwa watu moja kwa moja katika nyumba zao. Huduma hii inalenga moja kwa moja katika maeneo yanayojulikana kuwa na fahirisi ya juu ya uwezo wa kudhurika kijamii, inayoonyesha ukosefu wa usawa wa kiafya unaoweza kutokea. Watu wanaweza kuomba chanjo kupitia uchunguzi bila kujali mahali wanapoishi katika jimbo la Washington.

**Je, huduma nyingine za ndani ya nyumba zinapatikana zaidi ya chanjo ya COVID-19?**

Kwa sasa, timu za wauguzi wanaotembea tembea zinaweza tu kutoa chanjo za COVID-19. Chanjo ya mafua na huduma nyingine zinazoweza kutokea kama vile kutoa damu kwenye mahabara hazipatikani kwa wakati huu.

Huduma ya timu inayotembea tembea inapatikana ili kusaidia kuendeleza usawa wa watu wanaojulikana kuwa katika hatari ya juu ya kifo na kulazwa hospitalini kwa sababu ya COVID-19. Tafadhali zingatia kukamilisha uchunguzi huu kwa mtu anayehitaji ufikiaji wa chanjo ya COVID-19 leo.

**Naweza Kutarajia Nini Baada ya Kuwasilisha Ombi?**

DOH hukusanya fomu za ombi kila wiki na kuzituma kwa mamlaka ya afya ya ndani ya mkaazi kwa ajili ya ufikiaji na kitendo. Mhudumu wa ofisi ya afya ya ndani watafikia timu ya chanjo. Iwapo mhudumu wa afya ya ndani hawezi kuratibu chanjo ya wasioweza kutoka nyumbani, wataratibu na DOH ili kupata usaidizi.

Usaidizi wa laini ya lugha ya mbali unapatikana ili kusaidia mahitaji yoyote ya tafsiri. Iwapo ofisi ya afya ya umma ndani haiwezi kusaidia, ofisi inaweza kuomba usaidizi kutoka DOH. Timu ya usaidizi wa chanjo itashirikiana na mwombaji ili kuratibu huduma ya bila malipo ya COVID-19 ya watu wasioweza kutoka nyumbani.

**DOH 821-169 March 2022 Swahili**
Ili kuomba waraka huu katika muundo mwingine, piga simu 1-800-525-0127. Wateja ambao ni viziwi au wasio na uwezo wa kuzungumza, tafadhali piga simu 711 (Washington Relay) au tuma barua pepe civil.rights@doh.wa.gov.